HOTUBA YA MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA (MB), NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI NA UTAWALA BORA ALIYOITOA KWENYE MKUTANO NA WATUMISHI WA HALMASHAURI ZA WILAYA NA MJI MAGU TAREHE 03 OKTOBA, 2019

Mheshimiwa Dkt. Philemon Sengati, Mkuu wa Wilaya ya Magu,
Mstahiki Meya wa Mji Magu, Mheshimiwa Mwenyekiti wa
Halmashauri ya Wilaya Magu,
Mheshimiwa Balozi (Mstaafu) John M. Haule,
Mheshimiwa Khadija A. M. Mbarak,
Mheshimiwa Alhaj Yahya F. Mbila, Makamishna wa Tume,
Ndugu Nyakimura Muhoji, Katibu wa Tume,
Katibu Tawala wa Wilaya Mji Magu,
Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya na Mji Magu,
Watumishi wa Halmashauri za Wilaya na Mji Magu,
Waandishi wa Habari,
Mabibi na Mabwana,

Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya na kutuwezesha kukusanyika hapa leo ili kushiriki katika Kikao hiki cha kazi muhimu sana. Kwa namna ya kipekee kabisa, nawashukuru nyote kwa kuacha shughuli zenu na kuweza kufika mahali hapa. Lengo kuu la Kikao hiki ni kujifunza na kubadilishana uzoefu wa utendaji kazi katika Utumishi wa Umma.

Ndugu Watumishi wa Umma,

Azma ya Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni kuifikisha Tanzania kwenye Uchumi wa Kati kwa kutumia rasilimali tulizonazo nchini. Tanzania imejaaliwa rasilimali nyingi zikiwemo Rasilimali Watu, Rasilimali Fedha, Rasilimali Muda na Rasilimali Vitu ambazo zikisimamiwa kwa ukamilifu azma ya Serikali yetu itafikiwa pasipo shaka. Usimamizi na uendeshaji wa rasilimali nilizozitaja hapa juu unategemea sana Rasilimali Watu. Hivyo, nataka mfahamu umuhimu wenu katika kuchangia jitihada hizi za Serikali yetu ya Awamu ya Tano za kuelekea kwenye uchumi wa kati.

Ndugu Watumishi wa Umma,

Katika kuhakikisha azma hii ya Serikali inafikiwa, mnatakiwa kufanya kazi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma kwa kufanya kilicho sahihi huku mkizingatia Weledi, Uadilifu, Uaminifu na Uwajibikaji katika utendaji kazi wenu wa kila siku. Ili kuhakikisha kuwa mnatumia weledi katika utoaji wa huduma, mnafanya kazi kwa bidii, mnatumia Taarifa rasmi za kikazi na mnatoa huduma bora kwa wananchi wote bila upendeleo. Aidha, ili kuhakikisha kuwa mnatoa huduma bora kwa Umma, mnapaswa kuhakikisha mnatunza na kutumia ipasavyo dhamana mliyopewa kwa kuwajibika ipasavyo, kukamilisha majukumu yenu kwa wakati na kuheshimu sheria.

Ndugu Watumishi wa Umma,

Wote tunafahamu kuwa hakuna haki isiyo na wajibu. Kwa upande mmoja, Waajiri wana wajibu wa kuhakikisha watumishi wanapata stahili zao zote za kiutumishi ambazo ni haki yao, na kwa upande wa pili, watumishi wana wajibu wa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na tija. Hivyo, ni haki ya watumishi kupata stahiki zao mbalimbali za kiutumishi kama vile kupandishwa vyeo,

kuthibitishwa kazini na kulipwa stahili zao kwa wakati na kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma. Kwa ujumla, Watumishi wa Umma wana wajibu wa kufanya kazi kwa bidii, weledi, uadilifu, uaminifu na kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma.

Ndugu Watumishi wa Umma,

Utendaji kazi wenu wa kila siku ni lazima upimwe ili kupata tathmini ya utekelezaji wa malengo ya mtumishi mmoja mmoja na ya Taasisi kwa ujumla. Wote tunafahamu kuwa suala la ujazaji wa OPRAS ni takwa la kisheria kwa mujibu wa Kifungu cha **6** cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298. Hata hivyo, watumishi wengi wamekuwa hawajazi kabisa OPRAS au wamekuwa wakijaza kwa mazoea tu bila kuzingatia vipindi vya ujazaji, kuweka malengo ya utendaji kazi yasiyo "SMART" na kutokujaza fomu za OPRAS kwa ukamilifu. Kupitia Kikao hiki, ninaagiza kwamba, kila mtumishi ahakikishe kuwa anajaza OPRAS kikamilifu na kufanya tathmini ya utendaji kazi wake kama sheria inavyoelekeza.

Ndugu Watumishi wa Umma,

Jitihada za Serikali za kuhakikisha Utumishi wa Umma unazingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma, zinaenda sambamba na uchukuaji hatua za nidhamu kwa mujibu wa sheria dhidi ya Watumishi wanaokiuka maadili na miiko ya utendaji kazi. Watumishi wa Umma wana wajibu wa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma na kwa upande wa pili, wana haki ya kupata stahili zao kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma. Napenda niwahakikishie kuwa Serikali itaendelea kuweka mizania kati ya kutoa motisha kwa wale wanaozingatia kikamilifu maadili na kutoa ushauri na adhabu kwa wale wanaokiuka maadili kulingana na kiwango cha uzingatiaji au ukiukaji.

Hivyo, nasisitiza kuwa kila mmoja wenu hana budi kufahamu wajibu na haki zake kikamilifu na kuhakikisha kuwa anatekeleza kilicho sahihi kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma.

Ndugu Watumishi wa Umma,

Suala la watumishi kujiendeleza kielimu ni haki ya kila mtumishi lakini ni lazima lifanywe kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma. Natambua kuwa baadhi ya watumishi wamekuwa wakikiuka taratibu kwa kwenda masomoni bila ruhusa za Waajiri wao. Vitendo hivi vimesababisha watumishi wengi kupoteza ajira kwa kupatikana na hatia ya kosa la utoro. Kwa kupitia Kikao hiki, ninawataka watumishi wote kuzingatia taratibu zote zilizowekwa kuhusiana na mafunzo ikiwemo kuhakikisha kuwa wanaomba kuwekwa kwenye mipango ya mafunzo ya Taasisi zao na baadaye wanapata ruhusa ya kuhudhuria mafunzo husika.

Ndugu Watumishi wa Umma,

Mawasiliano ya barua ya mtumishi kwenda nje ya Taasisi yake ni lazima yafanyike kupitia kwa Mwajiri wake. Ni kinyume na utaratibu kwa mtumishi kuwasilisha barua yake nje ya Taasisi yake bila barua husika kupitishwa na Mwajiri wake. Watumishi watakaokiuka maelekezo haya ya kisheria watachukuliwa hatua za Nidhamu. Aidha, pale ambapo Mwajiri atagoma kupitisha barua ya mtumishi, basi mtumishi husika anaruhusiwa kuwasilisha barua yake mwenyewe akiambatanisha maelezo kuhusu Mwajiri wake kukataa kupitisha barua yake.

Ndugu Watumishi wa Umma,

Nichukue fursa hii pia kuwakumbusha kuhusu suala la utunzaji wa siri. Katika siku za hivi karibuni, tumeshuhudia mmomonyoko mkubwa wa maadili kwa

baadhi ya watumishi wa umma kuvujisha siri za Serikali. Nitumie Kikao hiki tena kuwataka watumishi wote wa umma kuzingatia viapo vyao vya maadili ya Utumishi wa Umma kwa ustawi wa nchi yetu. Serikali haitasita kuchukua hatua kali dhidi ya mtumishi yeyote atakayevujisha siri za Serikali.

Ndugu Watumishi wa Umma,

Matarajio ya Serikali ya Awamu ya Tano kwa Watumishi wa Umma ni kuwa na Watumishi walio na viwango vya juu kabisa vya nidhamu katika utendaji kazi; wanaojitolea kutoa huduma kwa Umma kwa moyo na bila upendeleo; wanaokamilisha majukumu yao kwa wakati, walio tayari kufanya kazi mahali popote; wanaowahi kazini; na wanaofanya kazi kwa kuzingatia Maadili ya Utumishi wa Umma. Aidha, Serikali kwa upande wake, itaendelea kuboresha maslahi ya watumishi na mazingira ya utendaji kazi kadri itakavyoweza na kwa kutegemea upatikanaji wa Rasilimali fedha.

INAWEZEKANA KUFANYA KAZI KWA KUZINGATIA SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA UTUMISHI WA UMMA. KILA MMOJA WETU ATEKELEZE WAJIBU WAKE.

AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA